



Ninapaswa kuwasiliana na nani ikiwa nina masuala kuhusu kesi yangu ambayo hayawezi kusuluhishwa na mtoa huduma za jamii wa FVS?

Ikiwa una suala au malalamiko kuhusu jinsi kesi yako inavyoshughulikiwa, wasiliana na msimamizi wa mtoa huduma wako wa jamii wa FVS. Ikiwa bado masuala yako hayajashughulikiwa, unaweza kuwasiliana na Msimamizi wa Eneo.

- Unaweza pia kupiga simu kwa Office of Constituent Relations (Ofisi ya Mahusiano ya Wahusika) kwa nambari 800-723-4831 au 360-902-8060 ili upate usaidizi wakati wowote, au unaweza kupiga simu kwa Office of the Family and Children's Ombuds (Ofisi ya Mpelelezi wa Malalamiko ya Masuala ya Familia na Watoto) kwa nambari 800-571-7321.

Ofisi ya Mpelelezi wa Malalamiko hupokea masuala na malalamiko kuhusu shughuli za Department of Children, Youth, and Families (Idara ya Watoto, Vijana na Familia). Ina mamlaka ya kuchunguza masuala.

Family Voluntary Services (Huduma za Kujitolea za Familia)

Kudumisha Usalama wa Watoto kwa Kuimarisha Familia



Washington State Department of
CHILDREN, YOUTH & FAMILIES

Family Voluntary Services (Huduma za Kujitolea za Familia, FVS) ni nini?

FVS ni mpango ambao unaruhusu wazazi kushiriki katika huduma za kutimiza mahitaji ya usalama, afya na ustawi wa watoto wao.

Lengo la FVS ni kudumisha usalama wa watoto na kutimiza mahitaji yao kwa kudumisha umoja wa familia. Unaweza kuamua kuacha kushiriki katika mpango wa FVS wakati wowote. Ukiamua kuacha kupokea huduma za FVS, Department of Children, Youth, and Families (Idara ya Watoto, Vijana na Familia, DCYF) itathmini kiwango cha usalama na hatari na kuamua iwapo inaweza kufunga kesi au kuwasilisha ombi la utegemezi.

Mambo ya kutarajia kutoka kwa mtoa huduma wako wa jamii wa FVS

- Kukuluhudumia wewe na watoto wako kwa heshima.
- Kushirikiana nawe na kuweka mpango wa kudumisha usalama wa watoto wako na kuhakikisha mahitaji ya watoto wako yanatimizwa.
- Kutoa huduma zinazokufaa wewe na familia yako.
- Kukutana na watoto nyumbani kwako kwa faragha mara moja hadi mbili kwa mwezi.
- Kukutana nawe angalau mara moja kwa mwezi nyumbani kwako, kwa kutoa taarifa au bila kutoa taarifa, ili kujadiliana kuhusu maendeleo na vizuizi.
- Kuwasiliana na watoa huduma, washirika wa jamii, familia na marafiki (kwa ruhusa yako) ili kupata mtazamo wa nje kuhusu maendeleo yako na ya familia yako.
- Kuzungumza nawe kuhusu suala la vurugu za kinyumbani na vigezo vingine vya hatari katika familia yako.
- Kukulimisha kuhusu usalama wa watoto wachanga panapohitajika.
- Ikiwa mtoto wako anashukiwa kunyanyaswa kingono kibiashara, kufanya utathmini wa hali na kutoa huduma zitakazosaidia.

Mambo ambayo mtoa huduma wako wa jamii wa FVS anatarajia kutoka kwako

- Kushiriki katika mchakato wa utathmini wa hali na kusaidia kubuni mpango wa kudumisha usalama wa watoto wako.
- Kufuata mpango wa usalama (iwapo upo).
- Kushiriki katika huduma za kudumisha usalama wa watoto wako na kupunguza hatari ya kunyanyaswa au kutelekezwa.
- Kuruhusu mtoa huduma za jamii wa FVS kukutana na watoto wako kwa faragha.
- Kukutana na mtoa huduma za jamii wa FVS mara kwa mara.
- Kuendelea kufahamisha mtoa huduma za jamii wa FVS kuhusu mabadiliko yoyote katika hali yako.
- Kutia sainsi ya kutolewa kwa maelezo yako na ya watoto wako.
- Kuhakikisha kwa heshima kuwa mtoa huduma za jamii anaelewa hali na mahitaji ya familia yako.



Mpango wa FVS hufanya kazi vipi?

Mpango wa FVS unaweza kutolewa ikiwa DCYF inachunguza familia yako kwa madai ya unyanyasaji wa watoto, kutelekezwa au tabia za hatari ya kiwango cha juu na:

- Kuna wasiwasi kuhusu uwezekano wa kutokea kwa hali ya unyanyasaji au utelekezaji wa watoto baadaye AU
- Kuna wasiwasi wa sasa kuhusu usalama wa mtoto wako.

Familia pia zinaweza kuomba huduma za FVS zinapohitajika kwa kupiga simu kwa DCYF.

